**SEKTA YA AFYA**

Wilaya ya Ileje imeendelea kujikita katika utekelezaji wa Ilani ya Chama Cha Mapinduzi na hasa katika kuhakikisha upatikanaji wa huduma bora ya afya hususani kwa wanawake, wazee na watoto. Katika kipindi hiki huduma za afya zimeboreshwa zaidi kwa kuongeza vituo vya kutolea huduma ya afya mpaka kufikia 43**,** hii inaonesha dhaili kuwa huduma ya afyaimewafikia wananchi wengi zaidi ukilinganisha na miaka ya nyuma. Jedwali lifuatalo linaonesha mchanganuo vituo vya afya vilivyopo

**Jedwali namba 14: Vituo vya kutolea huduma ya Afya Wilayani Ileje**

| **Na.** | **Vituo** | **Serikali** | **Binafsi** | **Taasisi** | **Jumla** |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. | Hospitali | 1 | 0 | 1 | 2 |
| 2 | Vituo vya Afya | 3 | 0 | 0 | 3 |
| 3. | Zahanati | 30 | 3 | 5 | 38 |
| 4. | Kliniki | 0 | 0 | 0 | 0 |
| **Jumla** | | **34** | **3** | **6** | **43** |

**Huduma za afya ya uzazi na Mtoto**

Wilaya ya Ileje ina jumla ya vituo 43 kati ya 43 ni vituo 40 vinavyotoa huduma za afya ya uzazi na mtoto yaani *RCH service.* Katika kipindi cha mwaka mmoja yaani 2022, idadi ya wajawazito waliohudhuria kliniki na kupewa huduma mbalimbali ni 12,313, Aidha vifo vya akinamama wajawazito hadi Disemba, 2022 vilikuwa 4.

Idadi ya akina mama wajawazito wanaohudhuria kliniki na kujifungulia katika vituo vya kutolea huduma za afya inaongezeka, katika kipindi cha mwaka 2021/22, mpaka kufikia Disemba 2022 watoto hai waliozaliwa walikuwa 3,361 ambapo vifo vya watoto wachanga vilikuwa **58 .**

**Huduma za chanjo kwa watoto chini ya miaka 5**

Wilaya ya Ileje imeendelea kufuata maagizo, miongozo na maelekezo ya Serikali ya kuhakikisha kwamba watoto wote wanapatiwa chanjo mbalimbali kadri inavyotakiwa, mpaka kufikia Disemba 2022 watoto jumla ya 3,426 kati ya walengwa 4,744 walipata chanjo sawa na 72.21% na zoezi la kutoa chanjo bado linaendelea, aidha kuongezeka kwa kiwango cha utoaji wa chanjo kimesaidia kudhibiti magonjwa ya mlipuko kwa watoto wa chini ya miaka 5, hivyo kupunguza vifo vya watoto chini ya miaka 5.

**Upatikanaji wa dawa na vifaa tiba Wilayani.**

**Mheshimiwa Waziri Mkuu;**

Upatikanaji wa dawa katika vituo vyote vya kutolea huduma kwa sasa ni nzuri kuliko wakati mwingine wowote kwani uko wastani wa 98.9%. Ili kuondoa usumbufu kwa wananchi, Wilaya imekuwa ikiomba kibali maalumu kutoka MSD na hivyo kununua dawa, vifaa tiba na vitenganishi vilivyokosekana katika bohari ya dawa, nje ya MSD kwa kutumia fedha za Mfuko wa Afya ya Jamii (iCHF), Bima ya Afya (NHIF), fedha za Papo kwa Papo (Userfee) pamoja na fedha za Mfuko wa Pamoja wa Afya (Basket Fund).

**Mfuko wa Afya ya Jamii (iCHF)**

Wilaya ya Ileje ina jumla ya kaya 80,708 aidha Halmashauri ina fanya hamasa, mashindano na kampeni mbalimbali katika kuhimiza wananchi kujiunga na Mfuko wa Afya ya Jamii (i-CHF) ambapo jumla ya Kaya 6,533 zimejiunga na CHF sawa na 8.1%

ya malengo ya wanachama 25,192 kufikia Disemba 2022. Wilaya inaendelea kuweka hamasa kwa viongozi wa kijamii, vijiji na wananchi kujiunga na i-CHF.

**11.5 Udhibiti wa Maambukizi ya UKIMWI**

Hali ya maabukizi ya UKIMWI Wilaya ya Ileje ni asilimia 4.9 ukilinganisha na Asilimia 5.6 ya Kimkoa. Pamoja na Serikali, Wilaya inajivunia uwepo wa taasisi zisizo za kiserikali ambazo zinaendelea kusaidia na kufanya kazi kwa pamoja katika kupambana na maambuki mapya ya VVU. Mashirika kama ***Walter Reed*** ni miongoni mwa wadau ambao wamechangia kuleta rasilimali watu na fedha katika kudhibiti UKIMWI.

Kwa kipindi cha Januari - Disemba, 2022 huduma za upimaji wa hiari na ushauri nasaha umeendelea kufanyika katika vituo ya huduma ambapo wateja 12,521walipimwa na kati yao wateja 235 walikutwa na maambukizi. Jumla ya wagonjwa waliokuwa katika dawa za kupunguza makali ya ugonjwa wa HIV ni 2756.

**Sera ya wazee na msamaha wa matibabu.**

Katika kuhakikisha sera ya matibabu bure kwa wazee inatekelezwa, Wilaya imetambua wazee 23,217 ambapo kwa mwaka fedha 2021/22 vitambulisho vya wazee 19,573 vimetengenezwa na kugawiwa kwa wahusika, hii ni mpaka kufikia Disemba 2022. Wilaya imeweka mikakati na ufuatiliaji endelevu wa kuhakikisha wazee wanapata matibabu kupitia dirisha lao maalum katika ngazi ya vituo vya afya na Hospitali.

**Ujenzi na ukarabati wa vituo vya kutolea huduma ya afya**.

Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Mhe. Dkt.Samia Suluhu Hassan Rais WA Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imeendelea kusogeza huduma za afya karibu zaidi na wananchi kwa kuimarisha na kuboresha miundombinu ya vituo vya kutolea huduma za afya. Aidha kwa kipindi cha Januari hadi Desemba 2022 Wilaya kupitia fedha za ruzuku, Mapato ya ndaniya Halmashauri na nguvu za wananchi imetumia Jumla ya **Tsh 2,861,341,215**kwa ajili ya ukarabati na ujenzi wa vituo vya kutolea huduma za afya pamoja na nyumba za watumishi wa afya. Jedwali namba 12 linaelezea zaidi.

**Jedwali kuonesha Fedha kwa ajili ya uboreshaji wa Miundombinu ya Afya na Ununuzi wa Dawa na Vifaa Tiba**

| **Halmashauri ya Wilaya ya Ileje** | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **Na** | **Miradi ya Afya** | **Hali ya Mradi** | **Kiasi cha Fedha (TZS)** | **Chanzo cha Fedha** |
| 2 | Ujenzi wa ICU Jengo la wagonjwa mahututi | Umekamilika | 250,000,000.00 | UVIKO |
| 3 | Ujenzi/Ukamilishaji wa zahanati 3 za Vijiji vya Yenzebwe,Kabale ,Shilinga,Ibezya na Mtima | Umaliziaji | 250,000,000.00 | Serikali kuu |
| 4 | Ujenzi wa Kituo cha afya Kata ya Itale | Umaliziaji | 500,000,000.00 | Serikali kuu |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | Ujenzi wa Kituo cha afya Kata ya Ndola | Umaliziaji | 500,000,000.00 | TOZO |
| 6 | Ukarabati Wa Isolation Ward | Ujenzi umeanza | 25,000,000.00 | Global Fund |
| 7 | Ujenzi wa Nyumba za watumishi 3 in 1 Kituo cha afya Lubanda | Ujenzi umekamilika | 90,000,000.00 | UVIKO |
| 8 | Ukamilishaji wa Ward tatu | Umaliziaji | 41,000,000 | Mapato ya ndani |
| 9 | Ujenzi wa DOT CENTRE | Umaliziaji | 55,341,215 | Global Fund |
| 10 | Ujenzi wa wodi 2 za Upasuaji (Me na Ke),Jengo la kuhifadhia Maiti pamoja na ukamilishaji wa jengo la Upasuaji,Mionzi na Maabara | Ujenzi unaendelea (Wodi 2)hatua ya umsingi na Mortury ujenzi upo katika hatua ya kupandisha kuta | 800,000,000 | Serikali kuu |
| 11 | Ununuzi wa Dawa na vifaa Tiba | Taratibu za manunuzi zinaendelea | 350,000,000 | Serikali kuu |
| **Jumla ndogo** | | | **2,861,341,215** | |

Fahari kubwa iliyopo kwa sasa ni kwamba Wilaya ya Ileje ina miradi ya ujenzi wa Hospitali, Vituo vya afya na zahanati mpya zinazojengwa na ziko katika hatua mbalimbali ndani ya Wilaya. Miradi hii ikikamilika itafanya Wilaya hii kuwa mojawapo ya Wilaya iliyofanikiwa kushawishi wananchi kujenga angalau Zahanati moja katika kila Kijiji kwa kutumia nguvu kazi za wananchi na fedha kutoka serikalini